JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA BABATI
SHULE YA SEKONDARI BABATI

S.L.P 126,
BABATI.
22/03/2022

MZAZI/ MLEZI WA ……..
S.L.P …….....
…….....…….....

YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BABATI - MANYARA

Tunakupongeza Kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari ya Babati Day,Mchepuo wa HGL/HKL Napenda kukujulisha kuwa shule itafunguliwa tarehe ..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ..... Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni siku za masomo.
Aidha utakapokuja shuleni lazima uwe na mahitaji yote yaliyoorodheshwa hapo chini.

1.1. ADA NA MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE KWA MUHULA.

I. Ada ya shule kwa Muhula mmoja ni Tsh……..35,000/=
2. Mchango wa ukarabati wa majengo na samani ni Tsh……20,000/= kwa muhula mmoja.
3. Fedha za tahadhari (hairudishwi) ni Tsh…….....5,000/=
4. Kitambulisho cha mwanafunzi na picha ni Tsh……...6,000/=
5. Mchango wa Taaluma kwa muhula ni Tsh. ……. 25,000/=
6. Mlinzi, mpishi na mhudumu kwa muhula ni Tsh …….…….....30,000/=
7. Nembo ya shule ni Tsh …….....2,000/=
8. Huduma ya Afya kwa Muhula kwa ajili ya usafiri tu ni Tsh .....5,000/=

JUMLA KUU NI TSH.....128,000/=

N.B. Malipo yote yanapaswa kufanyika katika Benki ya **NMB** kwa Akaunti Ifuatayo:- Babati day sekondari **A/C.No. 40701200117**. Unapaswa kuleta **Original Bank pay in slip** inayoonyesha jina la mwanafunzi, kidato na aina ya malipo **mfano:-** Ada ni Tsh 35,000/= Tahadhari ni Tsh 5,000/= n.k
(Hatutapokea fedha taslimu).

1:2. VIFAA VYA DARASANI.

1. Daftari za kutosha kubwa 10
2. Kalamu za wino na penseli.
3. Rula na kifutio.
4. Karatasi za photocopy (Ream 02(A_4).
5. Picha nne (4) passport size za rangi za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu.
6. Scientific calculator kwa mwanafunzi wa jiografia.

7. **VITABU**: Vitabu ni rasilimali muhimu sana kwa mwanafunzi kwani humpatia maarifa kamili juu ya masomo yake mbalimbali kwa wakati husika. Shule ina vitabu vichache, na itaendelea kununua vitabu kulingana na kasma itolewayo na serikali kuhusu kifungu hicho. Kila mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mtoto wake angalau nakala chache za vitabu kulingana na uwezo alionao mzazi.

VIFAA VYA USAFI NA VYOMBO VYA CHAKULA.

- Ndoo 2 za plastic za lita 20.
- Toilet brush (mabrashi ya kusafisha vyoo – mafupi na Fagio za brashi laini za kufagilia ndani.
- Drying mopper (squeezer) ya kudekia.
- Jembe moja (1)
- Kwanja
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

SARE YA SHULE:

Mzazi hakikisha mwanao ana:-

(i) Sketi mbili za kitambaa kizito rangi ya dark bluu (Zenye mshono wa rinda box toka juu hadi chini mbele na nyuma na kulia na kushoto marinda madogo ya kawaida) ziwe ndefu karibia na unyayo.
(ii) Mashati meupe mawili ya mikono mirefu (tetron), kwa wasichana wa kiislamu watavaa nusu kanzu na kitambaa cha kichwani cheupe chenye kufunika masikio na mabega (ushungi) usiwe na urembo - asinunue tai.
(iii) Neck tie (1) rangi ya sketi na pini moja.
(iv) Sweta dark blue lenye V.shep mbele.
(v) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufungua kamba na vyenye visigino vifupi.
(vi) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe.
(vii) T - Shirt pana, damu ya mzee (isiyo na maandishi) yenye kola.
(viii) Shamba dress sketi 1 kitambaa kizito rangi ya kahawia (brown) ya marinda ya kawaida ziwe ndefu karibia na unyayo (sample imeambatanishwa).
(ix) Raba za michezo (zenye kamba) na soksi ndefu rangi ya blue (stockings).
(x) Bukta na T-shirt (Jezi) ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo.
(xi) Tracksuit rangi nyeusi zenye ufito mweupe mikononi na miguuni.

Matandiko. (Ujinunulie)

xiv) Mashuka ya rangi ya light blue iliyoiva na pink iliyokolea na foronya zake.
xv) Mto (1)
xvi) Taulo
xvii) Kitenge au kanga 2 kwa ajili ya kuogea.
xviii) Neti nyeupe Square ‘4 x 4’
xix) Godoro lenye ‘cover’ ‘2½ x 6’
xx) Blanket moja.
xxi)Sanduku la chuma lenye kufuli (Tranker)

1.3 SHERIA ZA SHULE.

A: HESHIMA.

1) Wanafunzi wawe na heshima kwa waalimu, Wafanyakazi wote wa shule, wao kwa wao na mtu mwingine yeyote .
2) Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote wenyewe kwa wenyewe, kwa waalimu na watu wengine.
3) Wanafunzi wote hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo;

a) Kuvuta sigara, bangi na kutumia madawa ya kulevya kama mirungi mihadarati nk.

b) Kunywa pombe za aina yoyote.
c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama kofia, nguo fupi na za kubana.
d) Kugombana.
e) Kufuga ndevu
f) Kufuga kucha na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
g) Kunyoa kipara.
h) Kusuka nywele hairuhusiwi kabisa.

4) Wanafunzi wote ni lazima washirikiane na kusaidiana na waheshimu na wathamini kazi za aina zote.
5) Wanafunzi watatakiwa kuitikia mara moja na kukimbilia aliko mwalimu au kiongozi anayewaita, mara waitwapo.
6) Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha ya viongozi wa serikali wimbo wa Taifa, na fedha za Taifa.
7) Wanafunzi waheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule kutunza na kuthamini mali ya binafsi na mali ya umma.
8) Wanafunzi wawe mfano mzuri wa heshima mahali popote watakapokuwa.
9) Wanafunzi wawe kimya wakati wote wakiwa darasani wasitoke nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
10) Wanafunzi wanyooshe mikono juu na wasimame wanapouliza na kujibu swali.
11) Uhusiano kati ya wavulana na wasichana uwe wa kimasomo tu.
12) Kila mwanafunzi lazima ajue kuimba wimbo wa Taifa, wimbo wa uzalendo na wa shule.

B: MAHUDHURIO.

I) Ni lazima wanafunzi wote wahudhurie vipindi vyote vya masomo nje na ndani ya darasa.
ii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie kazi zote za mikono
iii) Wanafunzi wote ni lazima wahudhurie mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa n.k.

C: KUWAHI.

i) Wanafunzi wote ni lazima wawahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku kama vile vipindi vya darasani na nje ya darasa, wakati wa kurudi shule baada ya likizo, n.k.
ii) Wanafunzi ni lazima kuwahi haraka wanaposikia wito na dharura au kengele.

D: SARE ZA SHULE.

Ni lazima wanafunzi wote wavae sare za shule wakati wote wa:
a) Masomo ya darasani.
b) Wanapotoka nje ya shule.
c) Mhadhara wa shule (Baraza).
d) Wanapokwenda hospitalini.
e) Maandamano rasmi.
f) Kofia, viatu vya ghorofa , viatu vya wazi na mapambo yoyote hayaruhusiwi kuvaliwa na sare za shule.
g) Usafi wa sare na mavazi yote yaliyoruhusiwa shuleni lazima uzingatiwe kwa kila hali.
i) Wanafunzi wawe na kitambulisho na nembo ya shule kwenye mfuko wa shati la shule.

E: MIPAKA YA SHULE.

1. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya kibali / ruhusa ya maandishi na warudi kwa saa zilizoruhusiwa/pangwa.

2. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila ya kibali cha maandishi cha mwalimu.

i) Nyumba za waalimu na wafanyakazi wasio walimu.
ii) Vilabu vya pombe.
iii) Nyumba za starehe
iv) Nyumba za kufikia wageni.

NB. (ii), (iii) na (iv) hakuna ruhusa/ kibali kinachotolewa.

F: USAFI.

i. Kila mwanafunzi lazima azingatie usafi wa vifaa vyote wanavyotumia hapa shuleni na usafi wake binafsi (wa mwili)

ii) Kila mwanafunzi ni lazima awajibike kwa usafi wa mazingira ya shule. Ni marufuku kutupa karatasi ovyo, na ni marufuku kupita njia za vichochoro, kila mwanafunzi lazima atunze bustani za maua kwa kila hali.

1.4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi
(ii) Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(viii) Uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja au kuolewa.
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kama kunywa sumu n.k.
(xvi) uharibifu
(xvii) kutokufanya mitihani bila sababu za msingi.

MUHIMU (TANBIHI).

Adhabu kwa uvunjaji wa sheria za shule zitatolewa na Mwalimu wa Nidhamu, Baraza la Walimu, Bodi ya Shule au vyombo vingine vinavyohusika.

Kila mwanafunzi aje na cheti halisi cha kuzaliwa na Kivuli chake (Photocopy) pamoja na hati ya matokeo (result slip).

1.5 ANGALIZO.

i) Siku ya kufungua shule zoezi la ukaguzi litafanyika kikamilifu. Mwanafunzi ambaye atashindwa kutimiza mahitaji hayo hatapokelewa.

NB: Wanafunzi hawaruhusiwi;Kuja au kuletewa simu ya aina yoyote shuleni. Mawasiliano yote yapitie Ofisi ya Mkuu wa shule kwa,

- **Na. 0620-559531 - Mkuu wa shule.**
- **Na. 0784-293813 – Makamu mkuu wa shule**
- **Na. 0787-822838 – Makamu mkuu wa shule**
- **Na. 0786-171306 - Matron**
- **Na. 0784-427641** – **Mhasibu wa shule**

ii) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja au kuletewa aina yoyoye ya chakula shuleni.

iii) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na manukato wala vipodozi shuleni.

1.6 KUTEMBELEA WANAFUNZI

Mzazi/mlezi aliyesajiliwa na mwenye picha katika faili la mwanafunzi ndiye atakayeruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa sababu maalum katika siku za jumatatu hadi ijumaa kuanzia saa 8:30 mchana hadi saa 9:30 alasiri.

MWISHO: Ni matarajio yetu kuwa utaitumia vizuri nafasi hii ya pekee uliyopewa na serikali na utakuwa mfano mzuri wa **KITAALUMA, NIDHAMU, KAZI, USAFI, NA MICHEZO.**

Nakutakia mafanikio mema!

…….
PATRICK L. TARMO
MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA BABATI
SHULE YA SEKONDARI BABATI.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE.
FOMU HII IRUDISHWE SHULENI SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI IKIWA IMEJAZWA KIKAMILIFU.

1. A: MWANAFUNZI.

Mimi ……. nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule yako, pia sheria zake za shule kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninakubali/ninakataa nafasi hiyo na masharti ya shule na sheria zake kwa sababu ……
……
……..

Tarehe ……..... Sahihi ……

B: MZAZI/MLEZI.

Mimi ……...Mzazi/Mlezi wa ……. Ambaye amachaguliwa kujiunga na shule yako nimesoma maagizo na sheria zake. Ninakubali/ Ninakataa nafasi hiyo, ninaahidi/siahidi kumtimizia mtoto wangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na shule kwa muda uliopangwa.

Aidha, naahidi kushirikiana daima na uongozi wa shule katika kukuza, kumlea mtoto huyu kwa manufaa yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.

Kama ninakataa (Eleza sababu) …….
……
……

Ahsante.

Jina na anuani ya Mzazi / Mlezi. ……
……

Sahihi ……... Tarehe ……

(Futa lisilohusika).

NB: Sehemu ‘B’ Isainiwe na Mzazi/Mlezi na si vinginevyo

ORODHA YA VITABU UNAVYO WEZA KUJINUNULIA.

HISTORY.

1. A History of Modern Europe.
   1789 – 1981 By H. L. Peacock
2. Major events in the world History
- History paper 2 notes
- Advanced level F5 & F6
  By Gervas M. Zombe.
3. Major events in African Hist.
   By Jovitus F. Kamara Mweigage.
4. How Europe underdevelopment Africa.
   By Walter Rodney
5. Mastering African History in the world History up to 1945.
   By Mwl. Kato A. Gwampeewo.

ENGLISH.

English Advanced Learners' Dictionary Seventh/ Sixth Edition
By Oxford

Novels. 1) Encounters from Africa
2) His Excellency the Head of State "Danny Safo"
3. A season of Waiting "David omowale"
4. A man of the people "Chinua Achebe"
5. The beautiful ones are not yet Born. "Ayi Kwei Arruali"
6. Divine providence. Severin N. Ndunguru"
7. The Rape of the pearl "Magola Nyago"
8. Vanishing shadows "Namige Kayondo"

LIST OF PLAYS.

1. Betrayal in the City – "Fancis Imbaga"
2. I will marry when I want "Ngung'o and Ngusi Wa Mirii"
3. The bride – "Austriri Bukenya".
4. Iwanda Magere – "Ohoit Omtatah"
5. An Enemy of the people. – Henrik J. Bsen.
6. Black Mamba. – "John Rugamba"

POETRY.

1. Selected poems – Institute of education
2. The wonderful surgeon and other poems. "Charles Mloka".

A student should purchase at least two books in each category of Novel, Plays and Poetry. A dictionary is Compulsory for proper achievements.

- A dictionary which you are advised to buy is the Oxford Advanced Learners Dictionary.

GEOGRAPHY

1. Physical Geography by D.T Msabila
2. Geography in Diagrams for Africa by R.B. Bunett
3. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard
4. Human & Economic Geography (Advanced level paper 2) by D.T Msabila

5. Map Reading for East Africa by D. N. McMaster
6. Practical Geography (Map, Photo, statistics, survey& Research) for A. Level by Zisti Kamili
7. Research methology C.R.Kothari.
8. Principle of physical geography F.J Monkhouse

KISWAHILI

1. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita
2. Tahakiki – vitabu teule vya fasihi kidato cha tano na sita.
3. Riwaya
   - Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile
   - Kufikirika - Shaaban Robert
   - Mfadhili - Hussein Tuwa
   - Vuta N'kuvute – Shafii Adam Shafi
4. Tamthiliya
   - Kwenye Ukingo wa thim - Ebrahim Hussein
   - Morani – Emanuel Mbogo
   - Kivuli Kinaishi - Seif Mohamed
   - Nguzo Mama – Penina Muhando
5. Ushairi
   - Kimbuga - Haji Gora
   - Mapenzi Bora – Shaaban Robert
   - Chungu Tamu - Theobald A. Mvungi
   - Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu
6. Nadharia ya lugha ya Kiswahili 1 kidato cha 5 na sita.
7. Tafsiri na Ukalimani
8. Historia ya lugha ya Kiswahili.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA BABATI
SHULE YA SEKONDARI BABATI DAY

THE MEDICAL EXAMINATION FORM.

(To be completed by the Government Medical Officer and be returned to the school on registration day).

Pupil's name in full ……..……

Blood count (Red and White Blood cells) ……

Stool Examination ……..……

Urine analysis: ……..……

Syphilis Test: ……..……

T.B. Test: ……

Ears: ……..……

Chest: ……

Spleen: ……..……

Abdomen: ……...……

Pregnancy test……

Additional information e.g. physical Defects or Impairment infections, clinic or Family Diseases etc.
.....

DECLARATION:

I certify that the above mentioned pupil is fit to pursue his/ her further studies.
(If do not fit please state it clearly).....

Doctors Name.....

Doctor's signature.....

Date and Official Stamp.....